

TANGAZO KWA DIASPORA WOTE WA TANZANIA DUNIANI

Baraza la Diaspora wa Tanzania Duniani - Tanzania Global Diaspora Council linakutangazia kuanzishwa kwa kamati namba kumi ya Baraza - Kamati ya Sanaa, Utamaduni na Michezo. Baraza limeona umuhimu wa kuanzisha kamati hii na kuondoa majukumu haya ya Sanaa, Utamaduni na Michezo kutoka kamati namba tano – Kamati ya Vijana na kuyatengenezea kamati yake binafsi ili kuongeza tija na ufanisi, pia na kwa kuzingatia kuwa sio vijana tu ndio wanaoshughulika na Sanaa, Utamaduni na Michezo.

Kutokana na kuanzishwa kwa kamati hii ya Sanaa, Utamaduni na Michezo na kupitia tangazo hili. Kamati kuu ya TDC Global inawaomba Diaspora wote wenye nia ya kuiongoza kamati namba kumi kutuma maombi yao kwa barua pepe yetu ya huduma@tdcglobal.org

Muombaji ni lazima awe amejisajili katika Baraza kupitia tovuti ya Baraza <https://tdcglobal.org/member-register/> au www.tdcglobal.org

Katika barua pepe yako tuandikie yafuatayo:

1. Jina lako kamili
2. Namba yako ya simu ya kawaida na ya Whatsapp
3. Barua pepe yako itakayoweza kutumiwa na wanachama wetu(Diaspora) na Viongozi wengine na jamii kwa ujumla, pale watakapotaka kufanya mawasiliano na wewe.
4. Nchi unayotoka na address yako.
5. Kichwa cha habari andika maombi ya uongozi kamati ya Sanaa, Utamaduni na Michezo.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 05/10/2018. Tunatanguliza shukrani zetu kwa Diaspora wote kwa mnavyotupatia ushirikiano mzuri katika kujenga TDC Global imara kwa ajili ya kizazi hiki na kizazi kijacho. Kwa maelezo zaidi na ya haraka piga simu +4747262181.

Mungu awabariki sana

Nyagabona

Adolph N. Makaya

Katibu

Tanzania Global Diaspora Council.

2018-09-24

